Kila Neno La Upuzi

na

Ellis Forsman

Kila Neno La Upuzi

na

Ellis Forsman

Oktoba 7, 2011

Kila Neno La Upuzi

Math. 12:34-37

Viwango vya Mungu viko tofauti sana na vile vya dunia.

Isa. 55:8-9, *"Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu, asema BWANA. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu."*

Mfano wa kushangaza ya tofauti hii inategemea na mazungumzo ya mtu. Ulimwengu unachukulia kirahisi maneno fulani (inaruhusu mazungumzo ya aibu ikisema ni maneno huru). Wakati, Yesu alifundisha kuwa tuchukue kila neno tuki maanisha.

Math. 12:36-37, *"Basi nawambia kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu. Kwa kuwa kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa."*

Neno ni muhimu, kwa sababu inafunua moyo wa mtu. Math. 12:34, *"Enyi wazao wa nyoka mwawezaje kunena mema mkiwa wabaya? Maana kinywa cha mtu huyanena waujazayo moyo wake."*

Kwa hiyo maneno hufichua hakiba ya maneno iliyojificha katika moyo wa mwanadamu. Math. 12:35, *"Mtu mwema katika hakiba njema hutoa mema; na mtu mbaya katika hakiba mbaya."*

Kwa sababu hizi...

- Maneno yetu wenyewe yatapelekwa katika hesabu siku ya hukumu.
- Lazima tutowe mawazo mazuri kuhusu maneno tunayo zungumza.
- Ni vizuri kama maneno yetu yakiwa na kiwango cha Mungu na siyo dunia.

Katika somo hili, tuta tazama kile ambacho Biblia inafundisha kuhusu maneno yanayo kubalika na yasiyo kubalika. Tunaanza kwa kunyumbulisha maneno fulani ambayo yanalaaniwa na maandiko.

Maneno ya upuzi ambayo tutahukumiwa kwalo

Maneno ya upuzi – maneno yasiyo jenga. Gari ikiwa na upuzi haiwezi kusogea mbele.

Mfano wa kutokukubaliana maneno ya haraka: “Farasi manyoya!”

Mafano wa makubaliano maneno ya haraka: “Golly gee, ndiyo!” yote si sahihi.

Math. 5:37, *“Bali maneno yenu yawe ndiyo, ndiyo; siyo siyo kwa kuwa yazidiyo hayo yatoka kwa Yule mwovu.”*

Baadhi ya maneno ya mfano wa kawaida ya maneno yasiyokubalika.....

Kutumia jina la Bwana bure.

Kuto. 20:7, *“Usilitaje bure jina la BWANA Mungu wako, maana BWANA hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina lake bure.”*

Hiyo ni bila kuwa na tabia ya kweli ya marejeo. Mtu anaweza kuwa na hati katika njia mbili:

- Kutumia jina la Bwana katika kuapa au kulaani.
- Kutumia marudio ya upuzi kwa jina lake.

Hii pia inatumika katika jina la Yesu, kwa sababu jina lake litumike kwa heshima.

Wafil. 2: 9-11, *“Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTo NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba.”*

Maneno ambayo ni mabaya.

1 Petr. 3:10, *“Kwa maana atakaye kupenda maisha na kuona siku njema, auzuie ulimi wake usinene mabaya, na midomo yake isiseme hila.”*

Maneno ya uongo, au yale yanayo sababisha matatizo kati ya ndugu.

Mithali 6:16-19, *“Kuna vitusita anavyovichukia BWANA; Naam, viko saba vilivyo chukizo kwake. Macho ya kiburi, <u>ulimi wa uongo</u>, na mikono imwagayo damu isiyo na hatia; moyo uwazao mawazo mabaya; miguu iliyo myepesi kukimbilia maovu. <u>Shahidi wa uongo</u> <u>asemaye uongo</u>; naye apandaye mbegu za fitina kati ya ndugu.”*

Ulimi usemao uongo – 8267 angalia kitabu kiitwacho siyo ukweli; kilichoandikwa na a sham (inatangazwa maranyingi) kusema uongo. Uongo ili kuwasha moto. Mithali 11:18, *“Mtu mwovu hupata mshahara wa udanganyifu; apandaye haki atapata dhawabu ya hakika.”*

Kusema uongo – 3576 kazab – kudanganya (danganya). Maneno yasiyofa katika kusema uongo. Samsoni alimdanganya Delila kuhusu jinsi atakavyo wekwa kwa kufungwa na kamba mpya. Alishindwa kwa sababu ya maswali yake.

Swali, “Je naonekana nimenenepa?” Inaweza kusababisha uamzi unaofanana kwa mwanaume akitafuta jibu sahihi.

Maneno ya haki yanayo danganya.

Waru. 16:18, *“Kwa sababu walio hivyo hawamtumikii Bwana wetu Kristo, bali matumbo yao wenyewe, na kwa maneno laini na ya kujipendekeza waidanganya mioyo ya watu wanyofu.”*

Maneno ya haki – lugha iliyoundwa ili kudanganya; ukweli uvugu vugu.

Lugha chafu.

Waef. 5:4, *“Wala aibu, wala maneno ya upuzi, wala ubishi; hayo hayapendezi; bali afadhali kushukuru.”*

Mifano mingine ya lugha zisizo kubalika

Kutumia maneno kupita kiasi.

- Yakob. 1:26, *“Mtu akidhani ya kuwa anayo dini, wala hauzui ulimi wake kwa hatamu, hali akijidanganya moyo wake, dini yake mtu huyo haifai.”*
- Mith. 10:19, *“Katika wingi wa maneno hapakosi kuwa na maovu; bali yeye auzuiaye midomo yake hufanya hakili.”*
- Mith. 13:3, *“Yeye alindaye kinywa chake huilinda nafsi yake, bali afunuaye midomo yake atapata uharibifu.”*

Maneno yanayozungumzwa kwa kuhamaki.

- Mith. 29:20, *“Je umemwona mtu mwenye kuhamaki katika maneno? Afadhali kumtumaini mpumbavu kuliko yeye.”*
- Yakob. 1:19, *“Hayo mnajua ndugu zangu wapenzi. Basi kila mtu na awe mwepesi wa kusikia bali si mwepei wa kusema; wala kukasirika.”*

Kutawala ulimi unaweza ukawa mgumu, lakini Bwana anaonyesha kuwa itawezekana kama tukiifanyia kazi.

Kuongea uovu kwa wale walioko madarakani.

- Kutoka 22:28, *"Usimtukane Mungu wala usimlaani mkuu wa watu wako."*
- Yuda 1:8, *"Kadhalika na hawa katika kuota kwao huutia mwili uchafu, hukataa kutawaliwa, na kuyatukana matukufu."*

Kuongea uovu juu ya wale wanaotuzunguka.

Math. 5:21-22, *"Mmesikia watu wa kale walivyoambiwa, usiue na mtu akiua, itampasa hukumu. Bali mimi nawambieni, kila amwoneaye ndugu yake hasira itampasa hukumu na mtu akimfyolea ndugu yake, itampasa baraza; na mtu akimwapiza, itampasa jehanamu ya moto."*

"shenzi!; mjinga!" jina lingine lisilofaa.

Kauli kama hizo huitwa ya ovyo, na kwa uwazi zimepigwa marufuku.

1 Wakor. 6:9-10, *"Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawata urithi ufalme wa Mungu? Msidanganyike waasherati hawata urithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti, wala wezi, wala watamanio, wala walevi, wala watukanaji, wala wanyang'anyi.*

Maneno hewa.

Maneno ya bure nayo ni mfumo wa uongo. Ni maneno yanayosikika vizuri, lakini ni ya uongo, ikijaribu kumlainisha mtu kwa ajili ya msaada. Kwa mfano: "Unaonekana safi!"

- Zaburi 12:1-4, *"BWANA uokoe maana mcha Mungu amekoma maana waaminifu wametoweka katika binadamu. Husemezana yasiyofaa kila mtu na mwenziwe, wenye midomo ya kujipendekeza; husemezana kwa mioyo ya unafiki; BWANA ataikata midomo yote ya kujipendekeza, nao ulimi unenao maneno ya kiburi; waliosema kwa ndimi zetu tutashinda, midomo yetu ni yetu wenyewe, ni nani aliye bwana juu yetu?"*
- Waru. 16:18, *"Kwa sababu walio hivyo hawamtumikii Bwana wetu Kristo, bali matumbo yao wenyewe; na kwa maneno laini nay a kujipendekeza waidanganya mioyo ya watu wanyofu."*

Viapo vya haraka.

- Math. 5:33-37, *"Tena mmesikia watu wa kale walivyoambiwa, usiape uongo ila mtimizie Bwana nyapo zako; lakini mimi nawambia, usiape kabisa hata kwa mbingu, kwa maana ndicho kiti cha enzi cha Mungu; wala kwa nchi kwa maana ndiyo pa kuweka*

miguu yake; wala, wala kwa Yerusalemu, kwa maana ndiyo mji wa mfalme mkuu. Wala usiape kwa kichwa chako, maana huwezi kufanya unywele mmoja kuwa mweupe au mweusi. Bali maneno yenu yawe Ndiyo, ndiyo; Siyo siyo kwa kuwa yazidiyo hayo yatoka kwa yule mwovu."

- Yakobo 5:12*, "Lakini zaidi ya yote ndugu zangu, msiape wala kwa mbingu wala kwa nchi; wala kwa kiapo kinginecho chote, bali ndiyo yenu na iwe ndiyo, na siyo yenu iwe siyo, msije mkaangukia hukumu."*

Hiyo ndiyo maana mahakama yanamruhusu Mkristo kusema "Nathibitisha" badala ya "Naapa".

Neno lolote ambalo siyo zuri.

- Wakol. 3:8*, "Lakini sasa yawekeni mbali nanyi haya yote, hasira na ghadhabu, na uovu, na matukano, na matusi vinywani mwenu."*
- Waef. 4:29*, "Neno lolote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia."*

Hii inajumlisha maneno machafu (maneno ya kudhalilisha).

Mifano ya maneno hayo ni (kenge, mshenzi, kichwa bangi, nk).

Ni nini kibaya na matamshi haya? Yana maanisha kitu kile kile sawa na maneno mazuri yanayotumika kueleza kitu. Mfano kama, "Oh Mungu", "Yesu Kristo!"

Ni tendo baya inayoeleza hisia za maneno mabovu au yanafanana. Yanaonyesha tabia ya moyo tofauti na roho sahihi ya Mkristo.

- Waef. 4:31-32*, "Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matukano yaondoke kwenu, pamoja na kila namna ya ubaya; tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyo wasamehe ninyi."*
- Wakol. 3:8-15*, "Lakini sasa yawekeni mbali nanyi haya yote, hasira, na ghadhabu, na uovu, na matukano, na matusi vinywani mwenu. Msiambiane uongo, kwa kuwa mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake; mkivaa utu mpya, uanofanywa upya upate ufahamu sawasawa na mfano wake yeye aliyeuumba. Hapo hapana Myunani wala Myahudi, kutahiriwa wala kutokutahiriwa, mgeni wala mshenzi, mtumwa wala mwungwana, bali Kristo ni yote katika yote. Basi, kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao, jivikeni moyo wa rehema, utu wenu, unyenyekevu, upole, uvumilivu, , mkichukuliana na kusameheana mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake*

kama Bwana ninyi vivyo na ninyi. Zaidi ya hayo yote jivikeni upendo, ndio kifungo cha ukamilifu. Na amani ya Kristo iamue mioyoni mwenu; ndiyo mliyoitiwa katika mwili mmoja , tena iweni watu wa shukurani."

Mazungumzo yetu, ni moja ya tabia.....lakini tabia kama hiyo huonyesha *"Yaliyo mengi kwenye moyo"* , kile ambacho kimeruhusiwa kuwa ndani ya moyo na kufichua asili ya ukweli wa moyo kama ikitumika hivyo.

Nilikuwa na binamu ambaye asingeweza kusama neno bila kusema neno la kiapo. Katika maisha yake imekuwa ni tabia yake hawezi kuacha hiyo tabia. Math. 12:35

Tunapojaribu kutunza "*Hazina nzuri*" katika mioyo yetu, hapa kuna.....

Baadhi ya mbinu za mazungumzo yanayo kubalika

Maneno mawili ya muhimu ya muongozo:

Mazungumzo yetu yanapaswa kuongoza katika uelimishaji.

Waef. 4:29*, "Neno lolote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia."*

Ile inayotia moyo na kutujenga.

Ile inayosambaza neema kwa wengine.

Wakol. 4:6*, "Maneno yenu yawe na neema siku zote, yakikolea munyu mpatekujua jinsi iwapasavyo kumjibu kila mtu."*

Kwa mfano: maneno yanayo pooza mazungumzo ya juu. Mithali 15:1*, "Jawabu la upole hugeuza hasira, bali neno liumizalo huchochea ghadhabu.*

Mfano: maneno yalio na uvuvio kwa wale wanaosikia.

- Mithali. 15:4*, "Ulimi safi ni mti wa uzima; bali ukorofi wa ulimi huvunja moyo."*
- Mithali 15:23*, "Mtu hulifurahia jibu la kinywa chake; na neno linenwalo wakati wa kufaa ni jema kama nini."*
- Mithali 25:11*, "Neno linenwalo wakati wa kufaa ni kama machungwa katika vyanzo vya fedha."*

Maneno yetu lazima yawe na tabia ya kushukuru. Waef. 5:3-4, *"Lakini uasherati usitajwe kwenu kamwe, wala uchafu wowote wa kutamani, kama iwastahilivyo watakatifu; wala aibu wala maneno ya upuzi wala ubishi; hayo hayapendezi, bali afadhali kushukuru."*

Shukurani ni tabia ya watakatifu.

- Wakol. 1:12, *"Mkimshukuru Baba aliyewastahimilisha kupokea sehemu ya urithi wa watakatifu katika nuru."*
- Wakol. 2:7, *"Wenye shina na wenye kujengwa katika yeye, mmefanywa imara kwa imani kama mlivyofundishwa; mkizidi kutoa shukurani."*
- Wakol. 3:15, *"Na amani ya Kristo iamue mioyoni mwenu; ndiyo mliyoitiwa katika mwili mmoja, tana iweni watu wa shukurani."*
- Wakol. 3:17, *"Na kila mfanyalo kwa neno au kwa tendo fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye."*
- Wakol. 4:7, *"Tikiko ndugu mpendwa mtumishi mwaminifu, mjoli wangu katika Bwana atawaarifu mambo yangu yote."*

Kunung'unika na kulalamika siyo nzuri.

Wafil. 2:14-15, *"Yatendeni mambo yote pasipo manung'uniko wala mashindano, mpate kuwa wana wa Mungu wasio na lawama, wala udanganyifu, wasio na ila katika ya kizazi chenye ukaidi, kilichopotoka ambao kati ya hao manaonekana kuwa kama mianga katika ulimwengu."*

Hakuna mtu anayempenda mlalamikaji.

Mazungumzo yanayokubalika wakati mwingine yanahitaji kufikiriwa.

Mtu mwenye haki atatoa uangalifu mzuri wa mawazo yake katika mazungumzo.

Mithali 15:28, *"Moyo wa mwenye haki hufikiri jinsi atakavyojibu; bali kinywa cha wasio haki humwaga mabaya."*

Mtu mwenye haki atahusika na kile kinacho toka katika kinywa chake. Kwa sababu anajua kwamba mazungumzo yake yanaonyesha hali ya kweli ya moyo.

- Math. 12:34-35, *"Enyi wazao wa nyoka mwawezaje kunena mema, mkiwa wabaya? Maana kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake, mtu mwema katika akiba njema hutoa mema, na mtu mbaya katika akiba mbaya hutoa mabaya."*

- Math. 15:17-20, *"Hamjafahamu bado ya kuwa kila kiingiacho kinywani hupita tumboni, kikatupwa chooni? Bali vitokavyo kinywani vyatoka moyoni navyo ndivyo vimtiavyo mtu unajisi. Kwa maana moyoni hutoka mawazo mabaya, uuaji, uzinzi, uasherati, wivi, ushuhuda wa uongo na matukano; hayo ndiyo yamtiayo mtu unajisi; lakini kula kabisa hajanawa mikono hakumtii mtu unajisi."*

Anamtazamia Mungu kwa masaada, hata anakubali laana yaw engine.

Zaburi 141:3-4, *"Ee BWANA uweke mlinzi kinywani pangu, mngojezi mlangoni pa midomo yangu. Usiuelekeze moyo wangu kunako jambo baya, nisiyazoelee matendo yasiyofaa, pamoja na watu watendao maovu wala nisile vyakula vyao vya anasa."*

Mwisho

Imekuwa kusudi langu...

Kujikumbusha maneno ya Yesu katika:

Math. 12:36-37, *"Basi nawambia kila neno lisilo maana watakalolinena wanadamu watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu. Kwa kuwa kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa."*

Kuinua ufahamu wetu kwamba ni jinsi gani ilivyo rahisi kutenda dhambi katika mazungumzo yetu. Kujikumbusha kwa maneno ya neema ambayo yanaweza kutoka katika vinywa vyetu.

Nadhani nimeamsha fikira zako kutoa zingatio la umakini kwa viwango vya Mungu; kila mmoja wetu awe na nia kama ile iliyo tajwa katika sala ya mtunzi wa zaburi.

Zaburi 19:14, *"Maneno ya kinywa change, na mawazo ya moyo wangu, yapate kibali mbele zako Ee BWANA, mwamba wangu na mwokozi wangu."*